

OR – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

SHULE YA SEKONDARI MKWAMBA

S.L.P. 765, SUMBAWANGA

SIMU NA. 0755 053766

Tarehe:.....

Kumb.Na.MK WASS/JI.....

Ndugu:.....

**TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUINGIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha KWANZA mwaka wa masomo wa 2021 Unatakiwa kufika hapa shuleni tarehe \_\_\_\_\_. Shule inaumbali wa km kutoka Halmashauri.

Yafuatayo ni maelezo na maagizo ambayo unashauriwa kuyatumia kabla hujafika hapa shuleni.

**1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

- (i) Fika shuleni ukiwa na cheti cha kuzaliwa.
- (ii) Fika na Fomu ya kupimwa ikiwa imejazwa na Daktari wa serikali
- (iii) Fika na fomu hizo zikiwa zimejazwa kikamilifu na wahusika wote.

**2. SARE YA SHULE WAVULANA:**

- i. Anatakiwa awe na suruali mbili (NYEUSI NA KIJANI JESHI)
- ii. Mashati mawili (MEUPE) yenye mikono mifupi
- iii. Tai mbili (nyeusi na kijani jeshi)
- iv. Fulana(T-shirt) yenye nembo ya shule

**(Nguo hizi unaweza kujishonea au ukishindwa unaweza kuzipata shuleni)**

- v. Viatu jozi moja au zaidi visivyochongoka wala kuinuka mbele. Hivi viwe vya ngozi rangi nyeusi. Ndala hazitaruhusiwa kuvaliwa pamoja na sare ya shule.
- vi. Soksi fupi jozi mbili za rangi nyeusi na zisizo na mapambo yoyote.
- vii. Aje na mkanda mweusi wa ngozi wa suruali wenye “buckle” ndogo.
- viii. trakisuti kwa ajili ya michezo.(bluu)
- ix. Raba za michezo jozi moja (01)
- x. Aje na sweta (kijani jeshi) yenye shingo ya herufi „V”

**3. SARE YA WASICHANA**

- i. Sketi mbili (nyeusi na kijani jeshi)
  - ii. Mashati mawili (MEUPE) yenye mikono mifupi
  - iii. Tai mbili (nyeusi na kijani jeshi)
  - iv. Fulana(T-shirt) yenye nembo ya shule
- (Nguo hizi unaweza kujishonea au ukishindwa unaweza kuzipata shuleni)**

- v. Viatu jozi moja au zaidi visivyochongoka wala kuinuka mbele. Hivi viwe vya ngozi rangi nyeusi. Ndala hazitaruhusiwa kuvaliwa pamoja na sare ya shule.
- vi. Soksi fupi jozi mbili za rangi nyeupe na zisizo na mapambo yoyote.
- vii. gauni la kazi rangi ya bluu bahari
- viii. trakisuti kwa ajili ya michezo.(bluu)
- ix.Raba za michezo jozi moja (01)
- x. Aje na sweta (kijani jeshi) yenye shingo ya herufi „V”

#### 4. MAHITAJI MENGINE KWA WASICHANA WANAO KAA HOSTELI

- (i) Kila mwanafunzi awe na Sahani, Bakuli, Kikombe, Kijiko kwa ajili ya chakula.
- (ii) Lete Shuka mbili za pinki , blanketi moja, mto na Foronya mbili, pamoja na Chandarua. Vile vile ulete taulo moja ya kuogea na vifaa vingine vya usafi wa binafsi.
- iii) Ndoo 2 kwa ajili ya kutunzia maji na kuogea lita 10.
- (iv) Godoro moja lenye Inch (200 x 80) cm
- (v) pesa ya mpishi Tsh.80,000/= kwa mwaka
- (vi) mahindi debe 10 kwa mwaka
- (vii) maharage debe tatu 3 kwa mwaka

NB: Anaruhusiwa kutoa michango hii hata kwa kila robo ya muhula( mahindi, maharage na pesa)

#### 5. VIFAA MAALUMU KWA WASICHANA NA WAVULANA

- (i) Unatakiwa ulete Mathematical set (Mkebe wa vifaa vya Mahesabu) moja.
- (ii) Kwa upande wa masomo unatakiwa kuleta daftari kubwa (counter books) zisizopungua 12 kwa muhula za kutosha kuandikia katika masomo yako yote pamoja na” graph paper” pad moja na rim moja
- iii. Aje na kamusi (dictionary) ni muhimu na lazima
- iv. mfuko/ begi la mgongoni la kubebea daftari
- (v) Utakapofika hapa shuleni utasomewa sheria za shule na utaratibu mzima wa shule hii na utalazimika kuufuata. Ukikosa, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.
- (vi) aje na jembe jipya lenye mpini
- (vii) aje na ndoo moja lita kumi
- (viii) aje na .....

(IX)Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki “Simu au kifaa chochote kinachotumia umeme isipokuwa pasi tu”. Akipatikana na vitu hivyo atasimamishwa masomo au kufukuzwa shule na vifaa hivyo vitaharibiwa.

(X) Endapo mwanafunzi/mzazi/mlezi atakuwa na dharura awasiliane kwa kutumia simu ya shule.

7. Mwisho natumia fursa hii kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wote wa shule hii kukukaribisha hapa shuleni na naamini utatumia vizuri nafasi hii uliyopewa na Taifa ya kukuongezea elimu yako.

Karibu sana.

NB: NI HIARI KWA WASICHANA KUKAA HOSTEL KWA KIPINDI CHOTE CHA MASOMO NA PIA MZAZI/ MLEZI AMLETE MTOTO SHULENI  
Mkuu wa Shule,

LILIAN W. MWAKAFUNGA.  
SHULE YA SEKONDARI MKWAMBA  
SIMU YA MKONONI: 0755 053766  
Nakala kwa: Maafisa Elimu (W)

THE HEADMINISTRES  
MKWAMBA SECONDARY SCHOOL  
*Lilian W. Wakafunga*  
THE HEADMINISTRES  
MKWAMBA SECONDARY SCHOOL  
15/12/2020